**JAMUHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI**

SHULE YA SEKONDARI RUJEWA,
S.L.P. 133,
**RUJEWA.**

**06/12/ 2021**

**KUMB.NA.RJSS/JI/K.1/19/1/11.**

JINA LA MWANAFUNZI
…………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, shule ya sekondari **Rujewa** Mwaka **2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **24/01/2021**.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE YA SHULE

**(a) WAVULANA**

a) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi aina ya tetron.
b) Suruali mbili **damu ya mzee** zenye linda mbili kila pande, ziwe na turn up na zisiwe za kubana (**modal**).
c) Mkanda wa rangi **nyeusi** wa ngozi usio na picha wala maandishi/mapambo yoyote.
d) Tai mbili ya **damu ya mzee** ziwe za wastani (siyo ndefu sana wala fupi sana)
e) Viatu vya ngozi rangi **nyeusi** (vya kamba na visiwe vya **mchongoko** wala **kisigino kirefu)**
f) Soksi jozi**mbili nyeusi**
g) Sweta ya **kijani** shingo ya "V"

**(b) WASICHANA**

(a) Blauzi mbili (2) nyeupe za mikono mifupi aina ya tetron.
(b) Sketi mbili rangi **ya damu ya mzee** ndefu za linda box kitambaa kigumu (Zifike kifundo cha unyayo).
c) Tai mbili ya **damu ya mzee** ziwe za wastani (zisiwe ndefu sana wala fupi sana)
d) Viatu vya **ngozi rangi nyeusi** (vya kamba na visiwe vya mchongoko wala kisigino kirefu)
e) Soksi jozi mbili **nyeupe**
f) Sweta mbili ya **kijani** shingo ya "V"
g) Kwa waislamu watashona **nusu kanzu** nyeupe ambazo ni ndefu kidogo ikiambatana na **hijjabu (nyeupe)** ndefu kidogo.

2.2 Daftari kubwa (9), kalamu na mkebe wa hesabu

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wizara ya Elimu na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo utafafanuliwa utakaporipoti shuleni na nakala itabandikwa darasani ili uwe unajikumbusha mara kwa mara:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni muhimu
c ) Kutimiza/kutekeleza kwa makini maandalio ya jioni (preparations)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shulena nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wakohapa shuleni
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali ya umma.

## 3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

a) Wizi
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
c)Kugoma au kuhamasisha mgomo
d)Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu,walezi na jamii kwa ujumla
e)Kupigana na wanafunzi wenzake,kumpiga mwalimu, au mtu yeyote yule
f)Kusuka nywele , wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na **nywele fupi zizolingana sehemu zote wakati wote**
g) Kufuga ndevu .
h)Ulevi/unywaji wa pombe, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji sigara
i) Uasherati ,uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
j) Kupata ujauzito au kutoa mimba
k) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa, na matendo yeyote yanayovunja sheria za nchi
l)Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
m) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
**n)Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi** katika mazingira ya Shule
o)Kudharau bendera ya Taifa
p)Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu,nk
q)Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4.MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI SIKU YA KURIPOTI

(a) Medical examination form (Ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali).
(b) Fomu ya maelezo ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo nakadharika
(c) Tamko la mzazi

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**…………………….**

**MKUU WA SHULE**

**THE UNITED REPBULIK OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

RUJEWA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 133,
**RUJEWA.**
**06/12/2021**

To the medical officer I/C
………………………………………………………….
………………………………………………………….
…………………………………………………………..

Full name:......................………………………………………………………….
Age…………………………Years………………………Sex…………….…
Blood count (Red and White)……………………………………………………
Stool examination………...........................................................................................
Urine analysis……………………………………………….........................
Syphilis test………………………………………………………………..…
Eye test……………………………………………………………………....
T.B test……………………………………………………………..............
Ears……………………………………………………..................................
Chest……………………………………………………………………….
Spleen………………………………………………………………………
Abdomen…………………………………………………………...………
**ADDITIONAL INFORMATION** e.g. physical or chronically family disease,etc……………………………………………………………………...…
………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
I certify that the above named student is fit to pursue studies
Signature……………………………………………………………………
Designation…………………………………………………………………
Section………………………………………………………………………….
Date…………………………………………………………………………

**PUPILS:**
You must bring this complete form when you come to school, no student will be enrolled without certificate of physical fitness.

**……………………**
**HEAD OF SCHOOL**
**RUJEWA SECONDARY SCHOOL**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A**

(Ijazwe na Mwanafunzi)

JINA KAMILI...........................................................

Tarehe ya kuzaliwa......................Kabila...................Dini/Dhehebu......................

Shule ya msingi uliyosoma..........................................

Mahali unapoishi................................................ Mtaa.............................................

Jina la mwenyekiti wa mtaa ...............................................................

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI**

Jina la Baba/Mlezi.............................................................kazi yake.............................

Jinala Mama/Mlezi..............................................................kazi yake..............................

Wazazi/walezi wanaishi (wapi)....................................................pamoja au wametengana......................

Anwani ya mzazi/mlezi: S.L.P..............................................SIMU.............................

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi:

Sahihi ya Mwanafunzi..............................Tarehe................................

**KUKUBALI NAFASI (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe**)

Mimi..........................................................................Nimesoma maagizo na taratibu za Shule na Wizara kwa makini, na kuzielewa na nipo tayari kuzifuata,Hivyo nakubali nafasi niliyopewa na nitafika Shuleni siku/tarehe husika kama zilivyopangwa

Sahihi:............................Tarehe..........................

**KUTOSHIRIKI MGOMO /FUJO /MAKOSA YA JINAI**

(Ijazwe na mwanafunzimwenyewe)

**MIMI.............................................................................UMRI.............JINSI ME/KE……………**

**NAAHIDI** Kwamba nitakuwa mwadilifu na mwaminifu na kwamba sitashiriki wala kusababisha/kuchocheaMgomo kwa namna yeyote ile, na nitatoa taarifa kwa utawala pale nitakapoona viashiria vya mgomo/fujo au uvunjifu wa amani Shuleni .

Aidha naahidi kwamba hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa shule iwapo nitabainika kuwa nimeshiriki katika makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha sheria za shule na kifungu hiki

**SAHIHI......................................TAREHE......................................................**

**<u>SEHEMU B</u> :**

**FOMU YA MZAZI KUKIRI /KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZASHULE NA KUTOA MICHANGO YA VYAKULA NA MAHITAJI MENGINE YASHULE.**

**(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

MIMI.............................................................ambaye ni...................................................wa mwanafunzi huyu(uhusiano)……………………………………………

Nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na Sheria za Shule katika fomu ya kujiunga na shule na nipo tayari ajiunge na Shule hii, Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kikiwemo chakula cha shule ili aweze kupata Elimu yake vizuri katika Shule hii.

Aidha nitasaidiana nawalimu katika kumlea kijana huyu katika maadili mema, na kuitika wito wa kufika Shuleni pale nitakapohitajika.

Jina(mzazi/mlezi)................................................................

Anwani yangu ya kudumu ni.............................................SIMU....................................

Sahihi............................Tarehe......................